
# MUHTASARI WA SERA

## Wajibu wa Kimataifa, Uwajibikaji Ndani ya Nchi





Mkutano wa Mabadiliko ya Tabianchi wa Glasgow (COP26) unasisitiza k.m. 1) uharaka wa kulinda asili, ikijumuisha misitu, mandhari ya maji na mifumo ikolojia ya baharini na 2) haki za jamii za wenyeji na watu wa asili kuhusu ujuzi wao na kuishi kwa amani na asili yao. Sambamba na matokeo ya mkutano huo wa COP26, tunatoa wito kwa njia shirikishi na uundaji shirikishi wa maarifa kati ya utawala wa kiserikali na kikanda, sayansi na teknolojia, wadau wa ndani, na asasi za kiraia kulingana na uelewa wa muktadha ili kupunguza na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Kulingana na matokeo ya utafiti wetu na ushahidi unaotegemea uzoefu, tunapendekeza sera tatu kama ifuatavyo:

1. Njia shirikishi ya mara kwa mara ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi inatakiwa kuchukuliwa kama njia ya kukabiliana na udhaifu utokanao na hali ya hewa. **Njia shirikishi ni pamoja na michakato ya makusudi na jumuishi ya kijamii, uundaji wa maarifa kwa kushirikiana na jamii mahalia na ugawanaji wa rasilimali zinazohusiana na uhalali, ufadhili, vifaa na mtiririko wa habari katika jamii na jumuiya za mitaa.** Maendeleo ya kuwezesha majukwaa ili kuboresha ubadilishanaji habari yanahitajika. Majukwaa haya yanapaswa kutambua maarifa ya asili na kanuni za kitamaduni.

2. Mipango endelevu ya hiari na ya lazima ya uthibitishaji wa bidhaa na mazoea ya usimamizi vinapaswa kuwa shirikishi baina ya wadau na kuungwa mkono kupitia desturi za utawala uliyo rasmi na usiyo rasmi. **Kwa mfano, viwango vya uthibitisho na tathmini za athari za mazingira vinahitajika kushughulikia dhuluma na jinsi athari za kimazingira zinavyoingiliana, kwa mfano, na uporaji wa ardhi, haki za asili na mahitaji ya wenyeji.**

3. Ugumu wa matatizo yanayohusiana na mabadiliko ya tabianchi unahitaji njia za pamoja kuelekea mandhari, ambazo zinajaribu kupatanisha maslahi yanayokinzana na matumizi ya ardhi na kuoanisha mahitaji ya watu na asili. **Njia shirikishi za mpango wa mandhari zinapaswa kuwa jumuishi kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali kutoka katika ngazi, sekta, na taasisi mbalimbali** (kama vile serikali kuu na za mitaa, sekta za makampuni, masoko, sekta zisizo za kiserikali, taasisi za kidini, jamii za wenyeji) pamoja na kuziba pengo kati ya sekta mbalimbali.

   Aina hii ya njia shirikishi zinapaswa kuwezeshwa na kutengewa rasilimali. Michakato ya kufanya maamuzi inapaswa kuongozwa na kanuni za haki - ikijumuisha wazawa na jamii za wenyeji pamoja na mazingira na aina zisizo za kibinadamu, ambazo zote zinaingiliana na mazingira na msaada wa maisha.

2022

# MUHTASARI WA SERA

## Wajibu wa Kimataifa, Uwajibikaji Ndani ya Nchi







**Tangu mwaka 2012, utafiti wetu juu ya usimamizi wa maliasili nchini Ufini, Urusi, Msumbiji, Tanzania, Mexico na Indonesia umezingatia hasa uhusiano kati ya wadau kutoka ngazi mbalimbali, ushiriki wa umma, na mikakati ya usimamizi wa maliasili na uchukuaji hatua.**


**University of Eastern Finland, Finland**
Irmeli Mustalahti
Anna Mustonen
Denis Dobrynin
Ida Herdieckerhoff
Antti Erkkilä
Hanna Laako

**University of Lisbon, Portugal**
Rosário Oliveira

**College of Business Education, Tanzania**
Ubaldus J. Tumaini
Edda Tandi Lwoga

**The Law School of Tanzania, Dar es Salaam Tanzania**
Aristarik H. Maro

**Sokoine University of Agriculture, Tanzania**
Dismas Lyegendili Mwaseba

**Universitas Muhammadiyah Yogyakarta, Indonesia**
Rijal Ramdani
Eko Priyo Purnomo
Agustiyara
Aulia Nurkasiwi
Aqil Teguh Fathani

**Indonesian Palm Oil Association (GAPKI), Indonesia**
Agam Faturrochman

**Muhammadiyah Environmental Council, Indonesia**
Mohammad Nurcholis

**George Mason University, United State of America (USA)**
Kristina van Dexter



**Responsive Natural Resources Governance (RNRG) research group is funded by the Academy of Finland and the Finnish Strategic Research Council**
**irmeli.mustalahti(at)uef.fi**

https://sites.uef.fi/responsive-natural-resources-governance/

UNIVERSITY OF EASTERN FINLAND · UMY UNIVERSITAS MUHAMMADIYAH YOGYAKARTA · COLLEGE OF BUSINESS EDUCATION · Makutano · DEVELOP · ALL YOUTH · strategic RESEARCH